

Mambo ambayo Familia zilizo na Watoto Zinapaswa Kujua Kuhusu Chanjo za COVID-19

Tunaelewa kuwa watu wengi wana maswali kuhusu chanjo za COVID-19 kwa watoto wao. Hapo chini kuna majibu ya maswali ya kawaida ambayo wazazi na watunzaji wameuliza.

1. Chanjo za COVID-19 zinafundisha miili yetu jinsi ya kupambana na COVID-19 bila kutufanya tuugue.

Chanjo za COVID-19 huipa miili yetu onyesho la awali la jinsi virusi vya COVID-19 hufanya kazi ili mfumo wetu wa kinga uweze kuvitambua na kupambana navyo. Zinafanya hivi kwa kufundisha miili yetu jinsi ya kutengeneza protini mahususi za ugonjwa zinazoitwa kingamwili ili kutulinda. Chanjo za COVID-19 hazitupatii COVID-19.

Ingawa virusi vya COVID-19 ni vipya, wanasayansi wamekuwa wakichunguza aina za virusi hivi, vinavyojulikana kama virusi vya korona, kwa miongo kadhaa. Chanjo zote za COVID-19 zinazopatikana nchini Marekani zilipitia majaribio ya kimatibabu na kuidhinishwa kwa matumizi ya dharura na Mamlaka ya Vyakula na Dawa (FDA) ya Marekani. Zinapendekezwa na wataalam wa matibabu na afya ya umma kitaifa na hapa katika Vermont.

Mamilioni ya watu sasa wamepewa chanjo dhidi ya COVID-19 kwa usalama, wakiwemo watoto na vijana.

2. Baadhi ya watu wanaweza kuwa na athari zitokanazo

na chanjo, lakini kwa kawaida huwa kidogo na hazidumu kwa muda mrefu.

Chanjo imetengenezwa ili kuwapa watoto ulinzi wa kutosha na uwezekano mdogo wa athari za kimatibabu. Dozi ya chanjo kwa watoto ni kidogo kuliko dozi ya watu wenye umri wa miaka 12 na zaidi.

Watu wengine watakuwa na athari za kimatibabu kwa muda mfupi baada ya kupata chanjo, huku watu wengine hawatakuwa na hisia yoyote tofauti. Athari kutokana na chanjo za COVID-19 ni ishara za kawaida kwamba mwili wako unajenga kinga dhidi ya COVID-19. Athari za zinazoshuhudiwa sana ni: Maumivu kwenye mkono palipodungwa wakati wa kupata chanjo, homa, baridi na uchovu.

3. Kutopata chanjo kuna hatari zake kama vile ugonjwa sugu, matatizo ya moyo, na dalili zisizoisha.

Kutochanjwa kunaongeza hatari ya mtoto wako kupata ugonjwa kutokana na COVID-19. Watoto wengi watakata ugonjwa mwepesi tu, lakini baadhi yao watakuwa wagonjwa sana na hata kuhitaji kulazwa hospitalini.

Baadhi ya watu wanaouguwa COVID-19 wanaweza kuwa na dalili zisizoisha kwa muda mrefu (COVID ya muda mrefu). Dalili za kawaida za kudumu kwa watoto ni pamoja na uchovu, maumivu ya kichwa, kushindwa kulala, matatizo ya kuwa makini, maumivu ya misuli na viungo, na kikohozi.

Hatari ya kuvimba kwa moyo (uvimbe wa musuli wa moyo) ni kubwa kwa maambukizi ya COVID-19 kuliko kwa chanjo. Uvimbe wa musuli wa moyo unaweza kuwa athari nadra inayohusishwa na chanjo ya COVID-19, lakini kwa kawaida huishayenyewe bila matibabu.

Hali nadra lakini mbaya inayohusishwa na maambukizi ya COVID-19 kwa watoto husababisha uvimbe (kuvimba) katika viungo vyao uitwao ugonjwa wa uvimbe wa mifumo mingi, au MIS-C. Wanasayansi bado wanajifunza kuhusu MIS-C na jinsi inavyoathiri watoto.

Njia bora ya kumlinda mtoto wako ni kumsaidia kuzuia maambukizi ya COVID-19 — kupata chanjo, kuvaa barakoa bora na kuepuka sehemu zenye msongamano wa watu.

4. Kupata chanjo dhidi ya COVID-19 kuna manufaa.

Chanjo za COVID-19 zinaweza kupunguza hatari ya watu kueneza virusi vinyosababisha COVID-19. Kuhakikisha kwamba kila mtu anayestahiki amechanjwa kunaweza kusaidia familia nzima, ikiwemo ndugu ambao hawastahiki kupata chanjo na wanafamilia ambao wanaweza kuwa hatarini mwa kuugua sana wakiambukizwa.

Chanjo hutoa ulinzi bora kuliko maambukizi ya awali ya COVID-19. Watu ambao hawajachanjwa

ambao tayari walikuwa na COVID-19 wana uwezekano mkubwa wa kupata virusi tena kuliko watu ambao wamechanjwa kikamilifu.

Watoto walio Vermont wanapogunduliwa kuwa wana COVID-19, huathiri familia, mipango ya utunzaji wa watoto na shule. Kuwachanja watoto kutawalinda dhidi ya magonjwa hatari na kunaweza kusaidia kukomesha kuenea kwa COVID-19 katika jamii zetu.

Chanjo pia inamaanisha uhuru zaidi, ili watoto wa Vermont washiriki shughuli za watoto. Kunakuwa na wasiwasi mdogo kuhusu kutembelea marafiki na familia, kusafiri, na kwenda shuleni.

5. Unaweza kuwasaidia watoto wako wahisi wako tayari kupata chanjo zao za COVID-19.

Wazazi na watunzaji wanaweza kuchangia pakubwa katika kusaidia watoto kujihisi tayari kupata chanjo yoyote. Zungumza nao kuhusu mambo ya kutarajia wanapopata chanjo, na mambo yanayoweza kutokea katika siku zinazofuata. Huenda wakahisi kwamba wanaumwa kidogo kwa siku moja au mbili baada ya kupata chanjo yao, lakini haitadumu kwa muda mrefu.

Zungumza nao kuhusu jinsi chanjo itafundisha mwili wao kupambana na virusi vya COVID-19, na jinsi hatua ya kupata chanjo inasaidia kulinda kila mtu aliye karibu nao.

Maelezo zaidi kwa wazazi na watunzaji:

- Kupata Chanjo ya COVID-19 (Idara ya Afya ya Vermont): www.healthvermont.gov/MyVaccine | www.healthvermont.gov/KidsVaccine
- Sayansi Inayotumika katika Chanjo ya COVID-19: Maswali Yanayoulizwa Sana kwa Mzazi (Taasisi ya Wataalamu wa Watoto ya Marekani): www.healthychildren.org/English/health-issues/conditions/COVID-19/Pages/The-Science-Behind-the-COVID-19-Vaccine-Parent-FAQs.aspx

Januari 2022